

PRESS RELEASE

FOR IMMEDIATE RELEASE
November 28, 2017

Contact: Meg Muigai
mmuigai@iesc.org

JUKWAA LA KIDIJITALI LA MPANGO WA ENGINE UTAZISAIDIA BIASHARA NDOGONDOGO

Mpango wa Shirika la Feed the Future Tanzania wa Ustawishaji kupitia kwenye Uwekezaji na Ujasiriamali (ENGINE – Enabling Growth through Investment and Enterprise) ambao unafadhiliwa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) umezindua jukwaa la kidijitali la Bizfundi kwa minajili ya kutoa usaidizi kwa wajasiriamali na wafanyabiashara ndogondogo kwa kuwaunganisha na washauri na wakufunzi wa masuala ya biashara.

Naibu mkuu wa Mpango wa ENGINE na kiongozi wa kitengo cha Mitaji kwa Ustawishaji, Scott Bennett, anaelezea Bizfundi kama nyenzo ya kuzikutanisha biashara ndogondogo, za kadri na za kati (MSMEs) kwa upande mmoja na watoa huduma za ushauri wa biashara kwa upande mwingine. *“Jukwaa linaziwezesha wafanyabiashara waliojisajili kuwabaini kwa urahisi watoa huduma wenye ujuzi unaostahili wa kibiashara, kule ambako biashara zao ziko na kusaidiwa kuboresha utendaji na kukuza biashara zao,”* alisema Bennett.

“Jukwa hilo la kwenye mtandao pia litaziwezesha MSMEs kupata kwa urahisi zaidi taarifa, usaidizi na mitaji inayohitajika, wakati watoa huduma za ushauri wa biashara (business development service – BDS) na mashirika ya kifedha yataweza kunufaika na mtandao mkubwa zaidi wa wateja. Mpaka sasa jukwaa lina wamiliki wa biashara na watoa huduma za ushauri wa biashara karibu 200 waliojisajili.”

Jukwaa la kidijitali limeundwa chini ya kitengo cha ENGINE cha Mitaji kwa Ustawishaji, mradi wa miaka minne unaofadhiliwa na USAID. Jukwaa hilo hupatikana kwenye mtandao kupitia www.bizfundi.co.tz au kama app ya Android ambayo inaweza kupakuliwa kutoka Google Play store.

Mkuu wa kitengo cha ENGINE cha Uwezeshaji kwa Ustawishaji, Goodluck Mosha, amesema *“Bizfundi litalea ustawi na uwezo wa soko endelevu kwa watoa huduma za ushauri wa biashara kwa kuhakikisha MSMEs zinaweza kupata kwa urahisi usaidizi wa kuimarisha shughuli zao.”*

Feed the Future ni mpango wa serikali ya Marekani ya kukabiliana na masuala ya njaa na usalama wa chakula duniani. Ikiwa imewalenga zaidi wakulima wadogowadogo, hasa wanawake, Feed the Future inatoa usaidizi kwa nchi wabia wa kuendeleza sekta zao za kilimo ili kuchochea ustawi wa kiuchumi na kibiashara unaoongeza mapato na kupunguza njaa, umasikini na lishe duni.

USAID ndiyo wakala mkuu wa serikali ya Marekani inayoshughulikia kutokomeza umasikini uliokithiri na kuziwezesha jamii stahimilivu za kidemokrasia kufikia uwezo wao.

Kwa maelezo zaidi tembelea: www.feedthefuture.org, www.usaid.gov/tanzania, www.vegaalliance.org, au www.iesc.org.

###